# BARBRO JOHANSSON MODEL GIRLS' SECONDARY SCHOOL
## BARBRO GIRLS' SCHOOL

**P. O. Box 14556, Dar es Salaam, Tanzania. Tel: +255 (022) 2926482; (0) 757063349;**
**E-mail: Barbroschool@gmail.com; Website: www.johatrust.ac.tz**


……..…………2025

Wazazi /Walezi wa ………………………………………………………………………………..

**YAH: FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE KWA WANAFUNZI WAPYA / WAGENI WA MPANGO WA AWALI KABLA YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA ( PRE-FORM ONE)**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa binti yako amechaguliwa kujiunga na mpango wa awali kabla ya kuanza kidato cha kwanza (Pre Form One) katika Shule mfano ya Sekondari ya Wasichana ya Barbro Johansson (Shule ya Barbro). Hii ni Shule ya Wasichana ya bweni ambayo ipo katika kitongoji cha Luguruni katika Kata ya Kwembe, kilometa 28 kutoka mjini (Dar - es - Salaam).
Wanafunzi watakaojiunga na Pre - Form One wanatakiwa kuripoti shuleni siku ya Jumamosi, tarehe 04 Oktoba 2025, kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana.

Programu ya Mpango wa Awali (Pre - Form One) itaanza tarehe 04 Oktoba, 2025 hadi tarehe 05 Disemba, 2025. Mwishoni mwa Programu hiyo wanafunzi watafanya mitihani, wale wote watakaofaulu kwa wastani wa 50% watapewa fomu za kujiunga na shule moja kwa moja.

Binti yako atatakiwa kukamilisha taratibu zifuatazo kabla ya kusajiliwa shuleni tarehe 04 Oktoba 2025.

1. **Maelekezo**
Soma maelekezo kwa makini na ujaze hati ya kuridhia wajibu wa mwanafunzi wa Shule ya Barbro kisha uirejeshe hati hiyo shuleni. Unatakiwa kuelewa kwa makini vipengele vyote vya wajibu wa mwanafunzi wa Shule ya Barbro kabla ya kujaza na kuweka saini hati hiyo.

2. **Gharama za kusafiri**
Unawajibika kugharamia usafiri wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Tafadhali mpatie binti yako nauli ya kurudi nyumbani au itume shuleni kabla ya tarehe ya kufunga shule. Wanafunzi wanaosafiri kwenda mikoani wakati wa kufunga shule wapewe pesa za usafiri kutoka shuleni hadi kituo ambacho watapata usafiri wa mikoani. Shule haitahusika na gharama zozote za usafiri wa mwanafunzi.

Kalenda ya shule ambayo itakufahamisha matukio yote ya shule kwa mwaka 2025 imeambatanishwa.

3.***Malipo ya Ada ya Mpango wa awali kabla ya Kidato cha Kwanza***

Malipo ni Tshs. 470,000/=, malipo hayo ni lazima yafanyike kabla ya mwanafunzi kuripoti shule.

| MUDA WA MALIPO | KIASI | JINA LA AKAUNTI | NAMBA YA AKAUNTI | BENKI |
|---|---|---|---|---|
| Ada Kabla ya kuripoti Shuleni | 470,000/= | Barbro Johansson Model Girls' Secondary School | 01J1042999100 | CRDB |
| Pesa za kujikimu | 50,000 hadi 100,000 | Barbro Johansson Model Girls' Secondary School Shop, | 01J1042999102 | CRDB |

4. **Vifaa vinavyohitajika**

Shule itawapa wanafunzi mahitaji ya msingi kama vile godoro, vitabu vya kiada, ziada, na kadhalika. Mwanafunzi atatakiwa kuleta vitu vifuatavyo kutoka nyumbani na kuonyesha kwa mama mlezi/mwangalizi siku anaporipoti shuleni. Nguo na vifaa vyote vya mwanafunzi atakavyoleta kutoka nyumbani viwe na **alama ya jina lake, isiyofutika**, ili kurahisisha kuvitambua wakati vimechanganyika na vya wengine.

a. Nakala ya Matokeo ya Mtihani wa Mock wa Darasa la Saba
b. Nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.
c. Kalamu za wino za kuandikia na penseli
d. Madaftari madogo tisa (Exercise book) na Counter book mbili (quire 1)
e. Oxford Advanced Learner's Dictionary-International Student's Edition, latest edition inapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 46,000/=
f. Taulo – Iinapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 10,000/=
g. Jozi 1 ya kanda mbili - Zinapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 3,500/=
h. Shuka kwa kitanda cha ft..3 zisizopungua 4 zenye rangi ya bluu bahari na foronya 2, Shuka zinapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 14,000/= kwa shuka moja na foronya moja.
i. Chandarua cha kitanda cha ft. 3 ambacho kinapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 10,000/=.
j. Ndoo ya Lt. 10 ambayo pia inapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 5,000/=
k. Chanuo, mswaki, dawa ya meno, dawa ya viatu nyeusi (kiwi), brashi ya viatu
l. Mafuta na / au losheni ya ngozi
m. Mafuta ya nywele
n. Sabuni za kufulia na kuogea
o. Jozi isiyopungua moja ya khanga – Inapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 10,000
p. Taulo (pedi) za kike za kutosha kwa muhula wote. Zinapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 2,000/=
q. Chupi, sidiria na skin tight
r. Track suit 2 kwa ajili ya kuvaa wakati wa maandalizi ya jioni ambazo hupatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 35,000 kila moja
s. Nguo mbili za usiku (kulalia)
t. Sare 2 za kuvaa baada ya darasa ni gauni la miraba midogomidogo, lenye rangi ya damu ya mzee na nyeusi. Sare hizi zinalipiwa shuleni kwa bei ya shilingi 21,000/= kila moja.
u. Viatu vya darasani vya kutumbukiza vyeusi na raba za michezo nyeupe (picha ya aina ya viatu vinavyokubalika kwa darasani na raba za michezo imewekwa kwenye ukurasa wa 4)
v. Soksi nyeupe za darasani na michezo zisizopungua jozi nne (4). Zinapatikana pia kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 1,500/=
w. Jozi 1 ya viatu vya kawaida kwa ajili ya jumapili

x. Sweta ya bluu iliyokolea (dark blue) ambayo ni hiari. Sweta hupatikana pia katika duka la Shule kwa bei ya shilingi 20,000/=
y. Mto wa kulalia
z. Sare za shule alikotokea mwanafunzi kwa matumizi ya darasani
aa. Tochi au taa ya kutumia mionzi ya jua ambayo pia hupatikana kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 5,000/=
bb. Mwamvuli mdogo – ambao pia unapatikana kwenye dukala shule kwa bei ya shilingi 5,000/=
cc. Pasi ya umeme kwa ajili ya kunyooshea nguo. (Kila mwanafunzi atanyoosha nguo kwenye eneo maalum la kunyooshea kwa pasi yake binafsi).
dd. Sahani ya aluminium yenye sehemu za kuweka chakula na mboga na kijiko cha chakula, vyote hivi navyo hupatikana kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 5,500/=
ee. Kikombe cha chai na uji kisichovunjika kiurahisi, ambacho pia hupatikana kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 2,500/=
f.f Kadi ya bima ya afya kama anayo.

**Angalizo:-Wanafunzi hawaruhusiwi kuleta vyakula shuleni, nguo za nyumbani, vitu vya thamani kama vile kamera, redio, simu za mkononi na vitu vinavyoweza kusababisha ajali ya moto kama mishumaa, viberiti, taa za kandili n.k. kama ilivyofafanuliwa kwenye Wajibu wa Wanafunzi**.

5. **Huduma ya Afya**

Huduma ya kwanza inapatikana shuleni na zahanati ya karibu na shule iitwayo Luguruni. Tafadhali hakikisha mtoto wako anapimwa macho pamoja na afya kwa ujumla kabla ya kuripoti shuleni. Ikumbukwe kuwa mwanafunzi atapata huduma za msingi za tiba pindi akiugua shuleni, lakini shule haitahusika na matibabu ya magonjwa makubwa na sugu ya mwanafunzi ambayo yatakuwa ni jukumu la Wazazi/Walezi. Iwapo mwanafunzi ana kadi ya Bima ya afya aje nayo shuleni siku ya kuripoti na kuikabidhi kwa Mama Mlezi (Matron).

6. **Nidhamu**

Wanafunzi wote wanatakiwa kuzingatia au kutilia maanani wajibu wa mwanafunzi wa shule ya Barbro ambao umeambatanishwa. Kushindwa kufanya hivyo, kunaweza kusababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na mwanafunzi kusimamishwa shule au kufukuzwa shule.
Wanafunzi wote wanatakiwa kuwahi katika kila kitu, kuwa watiifu, wanaojituma, kuvumilia tofauti za wengine na kuonesha ushirikiano.

**Unakaribishwa sana katika Shule Mfano ya Sekondari ya Wasichana ya Barbro Johansson**




**Viatu vya darasani**

Viwe vyeusi  na vya kutumbukiza



**Raba za michezo**

Ziwe nyeupe na kufungwa kwa kamba